# KUMSWALIA MTUME

Kimeandikwa na:
**Sheikh Abdul Karim al-Bahbahani**

Kimetarjumiwa na:
**Sheikh Haroon Pingili**

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page B

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**

**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 17 - 001 - 2**

Kimeandikwa na:
**Shaikh Abdul Karim al-Bahbahani**

Kimetarjumiwa na:
**Shaikh Haroon Pingili**

Kimepangwa katika Kompyuta na:
**Hajat Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Januari,2011
**Nakala: 1000**

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**

**Alitrah Foundation**

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv.com

Katika mtandao: www.alitrah.info

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page C

# Yaliyomo

Neno la Jumuia……………………………………………………………7

Jinsi ya kumswalia Nabii (s.a.w.w.)...….………………………………11

Kumswalia Muhammad na Aali Muhammad kati ya Sunni na Shia….11

Sura ya kumswalia (s.a.w.w.)………………………………………......13

Al'Aali ni nani hao? .............................................................................. 16

Mas'ala hii ndani ya fiq'hi...…………...……………………………. ...18

Kilichochumwa na utafiti huu……....……………………………… …23

Faharasa………………………...……………………………………25

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page D



بسم الله الرحمن الرحيم

## NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho, *as-Swalaatu 'Ala 'n-Nabii,* kilichoandikwa na Sheikh Abdul Karim al-Bahahani. Sisi tumekiita, *Kumswalia Mtume.*

Kitabu hiki kinazungumzia juu ya hitilafu zilizotokea juu ya maneno yanayosomwa katika kumswalia Mtume Muhammad SAW *(**S**wallallaahu **'A**layhi **W**a-aalih).* Baadhi ya wanavyuoni wanasema kwamba kumswalia Mtume ni kusema: *"Allaahumma swalli 'alaa Muhammad"* bila kuongeza kitu. Wengine wanasema kumswalia Mtume ni kusema: *"Allaahumma swalli 'alaa Muhammad wa Aali Muhammad"* kama utakaavyoona maelezo yake ndani ya kitabu hiki.

Sheikh wetu huyu amefanya utafiti wa kina juu ya suala hili na kuonyesha kwa uwazi na pasina shaka yoyote juu ya asili ya swala ya Mtukufu Mtume. Mwanachuoni huyu mtafiti ametumia vyanzo halisi na sahihi katika kulifikia lengo lake hili. Vyanzo hivyo si vingine bali ni Qur'ani na Sunna, pamoja na matukio ya kweli ya kihistoria, akili, mantiki na elimu.

Kutokana na umuhimu wa maudhui hii tumeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ili kutoa mwanga kwa Waislamu wazungumzaji wa Kiswahili juu ya suala hili ambalo linawatatiza na kujua ukweli wake.

Tunamshukuru ndugu yetu Sheikh Haroon Pingili kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote ambao wameshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page E




Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa chenye manufaa sana kwa wasomaji wetu na kuzidisha elimu yao ya dini.

Mchapishaji
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701, Dar-es-Salaam.

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page F

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page 1



kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page 2



# KUMSWALIA NABII (s.a.w.w.)

## NENO LA JUMUIA

Kwa kweli urithi wa Ahlul-Bayt (a.s.) uliohifadhiwa na madrasa yao na wafuasi wao kuulinda usipotee wadhihirisha kuwa ni madrasa yenye kukusanya matawi mbalimbali ya maarifa ya kiislamu.

Na madrasa hii imeweza kuzilea nafsi zilizojiandaa kuteka kutoka maji haya safi, na kuupatia umma wa kiislamu wanazuoni wa kubwa wafuatao nyayo za ki-risala za Ahlul-Bayt (a.s.) wenye kuzichukua chochezi zote na mas'ala mbalimbali ya kimadhehebu na mielekeo ya kifikra ndani na nje ya maisha ya kileo ya kiislamu. Wakiipa majibu yaliyo madhubuti na ufumbuzi muda wote wa karne zinazofuatia.

***Majmaul'a'lamii*** ya Ahlul-Bayt imeharakia – ikianzia majukumu yake iliyojibebesha mabegani mwake – ili kuilinda heshma ya risala isiyoweza kukiukwa, na hakika zake ambazo zimetiwa ukungu na wanavikundi na madhehebu na watu wa mielekeo inayopingana na Uislam, ikifuata nyayo za Ahlul-Bayt a.s. na wafuasi wa madrasa yao ongofu ambayo imepupia kuujibu uchochezi unaoendelea, na imejaribu kubakia daima mbele ya msitari wa mapambano kwa kiwango kinachotakiwa katika kila zama.

Kwa kweli uzoefu unaohifadhiwa na vitabu vya wanazuoni wa madrasa ya Ahlul-Bayt (a.s.) katika lengo hili ni wa aina ya pekee; kwa sababu una akiba ya elimu inayohukumika kwenye mahakama ya akili na thibitisho na unajiepusha na uchu na upendeleo ulaumiwao, na unawasemesha wanazuoni na wanafikra waliobobea semesho ikubalikayo na akili na kupokelewa vyema na umbile lililosalama. Na limekuja jaribio la ***Al-majmau'alamiy*** ya Ahlul-Bayt (a.s.) ili iwape watafutao ukweli daraja mpya ya uzoefu huu ulio tajiri katika uwanja wa mazungumzo na kuuliza na

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page 3



kuzipatia majibu shub'ha – zilizochochewa katika zama zilizopita au zinazochochewa hii leo na khaaswa kwa kusaidiwa na baadhi ya duru zenye hikdi dhidi ya Uislam na Waislamu kupitia vyombo vya habari vya internet na vingine – ikijiepusha mbali na uchochezi ulaumiwao ikiwa na pupa kuzitia chachu akili zenye kufikiri na nafsi zitafutazo ukweli, ili zifungukiwe na ukweli unaotolewa na madrasa ya kirisala ya Ahlul-Bayt kwa ulimwengu wote, katika wakati ambao akili zinakomaa na nafsi na roho zinawasiliana kwa haraka mno na kwa namna ya pekee.

Hapana budi tuashirie kuwa kundi hili la utafiti limeandaliwa katika kamati makhsusi ya kundi la watukufu. Na tunatoa shukrani nyingi kwa wote hao na kwa walio na ubora na uhakiki kwa kufanya rejea kwao wote hao sehemu ya utafiti huu na kudhihirisha maoni yao ya maana kuhusiana nayo.

Na sote tuna matumaini na matarajio tuwe tumetoa tuwezalo miongoni mwa juhudi ya kutekeleza baadhi ya ambayo ni wajibu juu yetu kuielekea risala ya Mola wetu mtukufu Ambaye amemtuma Mtume Wake kwa uongofu na dini ya haki ili izishinde dini zote na Mungu ni shahidi tosha.

**JUMUIYA YA KIMATAIFA YA AHLUL-BAITI**
**KITENGO CHA UTAMADUNI**

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page 4



# كيفية الصلاة على النبي صلى الله عليه وأله

**Jinsi ya kumswalia Nabii (s.a.w.w.)**

# الصلاة على محمد وأله بين السنة والشيعة

**Kumswalia Muhammad na Aali zake kati ya Wafuasi wa madhehebu ya Sunni na wa Shia**

Mas'ala ya kumswalia Nabii yanazingatiwa kuwa ni katika jumla ya mas'ala ambazo Waislamu wameafikiana juu ya asili ya kuwepo kwake na wamehitilafiana katika ufafanuzi na jinsi ya utekelezwaji wake.

Ama asili ya mas'ala hii ni ile kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

﴿ إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلَٰٓئِكَتَهُۥ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِيِّ ۚ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ صَلُّوا۟ عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا۟ تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾ ﴾

**"Kwa hakika Mwenye enzi Mungu na malaika wake wanamtakia rehma Nabii. Enyi mlioamini, mtakiyeni rehma yeye na msalimieni sana." (*Al'Ahzab* : 56).**

Aya hii inashirikiana na Aya nyingine ambayo imeashiria kwenye utakiaji rehma wa Mungu (s.w.t.) kwa ajili ya waja wake.

Mfano wa kauli Yake (s.w.t.):

﴿ هُوَ ٱلَّذِى يُصَلِّى عَلَيْكُمْ وَمَلَٰٓئِكَتُهُۥ لِيُخْرِجَكُم مِّنَ ٱلظُّلُمَٰتِ إِلَى ٱلنُّورِ ۚ وَكَانَ بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَحِيمًا ﴿٤٣﴾ ﴾

**"Yeye ndiye ambaye anakutakieni rehma na malaika wake ili akutoeni gizani na kukupelekeni kwenye nuru, na Yeye ni mrehemevu mno kwa waumini. (*Al'Ahzab* : 43).**

*Swala kutoka kwa Mungu kuwaendea waumini maana yake ni maghfira na rehma, na kutoka kwa asiyekuwa Mungu maana yake ni dua ya kuomba ghufrani na rehma.

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page 5



Na Aya ya tatu imeashiria kwenye swala ya Nabii kwa baadhi ya waumini, nayo ni kauli yake (s.w.t.):

﴿ خُذْ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِم بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ۖ إِنَّ صَلَوٰتَكَ سَكَنٌ لَّهُمْ ۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ (١٠٣) ﴾

**"Chukuwa swadaqa kutoka mali zao utakuwa unawatoharisha na kuwatakasa kwazo, na waombee maghufra na rehma, kwa kuwa kuwaombea kwako ghofrani na rehema ni utulivu kwao na Mwenyezi Mungu ni Msikivu, Mjuzi mno." (*At-Tawba*:103).**

Wafasiri wengi wameashiria kuwa swala ya mja kwa Mola wake ni dua na kumuadhimisha; na swala ya Mwenyezi Mungu kwa mja wake ni rehma na takrima kwa dalili ya sababu iliyoelezwa:

**ليخرجكم من الظلمات الى النور وكان بالمؤ منين رحيما"**

"Ili akutoeni gizani muende kwenye nuru, na yu mwingi wa rehma kwa waumini."

Na swala ya Rasuul kwa waumini ni dua ya kheri kwa ajili yao na baraka. Na swala ya malaika kwa Rasuul au kwa waumini ni dua na ***istighfaar.*** [1]

Na Swala hii ya kubadilishana kati ya mja na Mola na Rasuul, Swala ya mja kwa ajili ya Mola, na Swala ya Mola kwa ajili ya mja na swala ya Rasuul kwa ajili ya waumini, na swala ya waumini kwa ajili ya Rasuul, inafanya sura kamili mno ya mshikamano na muambatano kati ya muumba na kiumbe, kati ya umma na Raisi wake. Ili kila upande ujue nafasi yake na daraja ya upande ule ambao yeye yuko mbele yake, wala mipaka haipotei kwenye mikunjo ya mshikamano huu. Hivyo mja huswali kwa ajili ya taadhima na kutekeleza haki ya uja na utumwa kwa Muumba mtukufu.

**1. *Al'Miizan :* 9 : 398. 16 : 335. Pia angalia: *Tafsyirul'Kabiir* 16 : 180, 25 : 215, 227.**

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:45 AM Page 6



Na Mwenyezi Mungu anaswalia kwa kumpa heshma na sharafu na kumrehemu huyu mja mtambuzi. Na mu'umini anamswalia Rasuul kutambua daraja yake na kusalimu amri ya uwalii wake, na Mtume humswalia muumini kumpa heshma na kumtakia ziyada ya kheri kwa ajili yake.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amemfanya Nabii wake kuwa makhsusi kwa daraja za juu mno za heshma na usharifu kwa ajili yake, pale alipomswalia na malaika wake wakamswalia, na kuwalazimisha waumini wamswalie. Na imekuwa miongoni mwa heshima hizo ni umma wake ambao umemuamini na kuzitii amri zake. Hivyo ikawa swala ya Mungu na malaika wake na mjumbe wake ni sehemu za heshma ile na ni dondoo kutoka kwenye kishubaka kile na ni kitu mahsusi umma huu hutambulika kwacho mbali na umma zingine zilizokuja kabla yake.

## صيغة الصلاة على النبي صل الله عليه وأله وسلم

## Sura ya swala ya Nabii (s.a.w.w.)

Wanazuoni wa madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) wameafikiana kuwa haitoshi kumtaja Nabii (s.a.w.w.) peke yake katika swala bali ni wajibu kuwataja Aali zake pamoja na yeye. [2]

Wakitoa dalili kuthibitisha hilo kwa habari (mapokezi yake) ni ya kata shauri zilizokuja kutoka urithi wa pande zote mbili.

Mfano wa habari *mashuri* kutoka vyanzo vya kisunni [3]

2 *Al'Khilafu li-Sheikh Tusi* Juz. 1, uk. 373. *Tadhkiratul'fuqaha'u* Juz. 3, uk. 233. Na *Jawahirul-kalaam* Juz. 10, uk. 261.

3 Nayo ni Salaamu ya tashahud katika swala, ilikuwa tokea hapo mwanzo. Nayo sio salam na swala na khasa ile ya baada yake: *swala llahu alayhi wa salam,* hii ni miongoni mwa yasiyokuwa na dalili. Na Aya: وسلموا تسليما hapana katika habari kutoka kwa maimamu walio tohara (a.s.) ila hii ni taslimu ya utii sio taslimu ya kusalimia kama tafsiri yake ilivyokuja ndani ya *Tafsirul-Ayyashiy* na ya al'Qummiy. Angalia Maqalata: "وسلموا تسليما انقيادا أو تكريما؟" فى العدد 15
15 *Majalatul'fikril'islamiy lil'Yusifu al'Gharawey*.

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 7



"Kuwa Nabii (s.a.w.w.) alitujia tukasema: Ewe Mtume wa Mungu tumejua jinsi ya kukusalimia, vipi tutakuswalia?

Akasema: Semeni:

**اللهم صلى على محمد وعلى ال محمد كما صليت على ابرا هيم انك حميدمجيد**

*Allahumma swali ala Muhammadin wa ala Aali Muhammad kama swalayta ala Ibraahiima Innaka hamiidun majiidun.* [4]

Na Nassu mfano wa hii wameileta baadhi ya wafasiri wengine kwenye Aya hii: ان الله وملا ئكته يصلون على النبي.. (*al'Ahzab*:56) na katika tamko la mkato na msisitizo fuatilia Ibn Hajar alipoeleza ndani ya *Sawaiqu al'-muhriqah* kuwa yeye s.a.w alisema:

**:لا تصلوا علي الصلاة البتراء. فقالوا: وما الصلاة البتراء؟ قال: تقولون اللهم صلى على محمد وتسكتون, بل قولوا: اللهم صلى على محمد وعلى أل محمد)**

"Msiniswalie swala iliokatwa." Wakasema: "Swala iliyokatwa ni swala gani?" Akanena: "Munasema: *Allahumma Swali ala Muhammadin* na mwanyamaza, bali semeni: Allahumma Swali ala Muhammad wa ala Aali Muhammad. [5]

Japokuwa dalili hizi ni nyingi na zipo kwa mkazo wa kuwakusanya - ndani ya swala - kati ya Nabii na Aali zake, ila tu ni kwamba fiqhi ya kisunni haikukata shauri la kuwaswalia Aali Muhammad. Kuna aliyewajibisha kuwataja Aali Muhammad katika kumswalia na kuna asiye wajibisha [6] Akitoa hoja kwa sababu duni, kalamu yenye hadhi inajiepusha kuzitaja

4. *Swahihul-Bukhariy*, Juz. 6, uk. 217 Hadithi ya. 291. *Sunanut 'Tirmidhiy* Juz. 5 uk. 359 H. 32. **والحديث متفق عليه.**

5. *al'Swawaiqu al'muhriqah*: 225. Chapa ya.Beirut.

6. *Al'Majmu'u lil'Imamun Nawawiy* Juz. 3, uk. 466 – 467.

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 8



sembuse kuziamini. Mfano wa kauli yake: Kuwa kutokuwa wajibu ni bora kwa kuwa Nabii (s.a.w.w.) aliwaamrisha hilo - yaani kuwataja Aali pamwe na Nabii (s.a.w.w.) walipomuuliza awaelimishe hakuanza yeye – kuwajulisha hilo. [7]

Jibu la hoja hiyo ni: Kuwa Nabii (s.a.w.w.) alikuwa - wakati mwingine – yuatosheka na kumuuliza kwao ili kuieleza hukumu kwao inayoambatana na maudhui ya mas'ala, na lau wasingemuuliza angeharakia kuieleza hukumu hii ya kisheria. Na hali kama hii ina mifano mingi ya Qur'ani. Qur'an tukufu imeileta kwa anuwani: (***Yas'aluunaka***), kama mfano uliopo katika:

"يسأ لونك عن المحيض" = Wanakuuliza kuhusu wenye hedhi.

' يسأ لونك عن الشهر الحرام" = Wanakuuliza kuhusu miezi mitukufu.

يسأ لونك عن الخمر والميسر' = Wanakuuliza kuhusu pombe na kamari.

Na mengine, kwa hiyo kulingana na madai haya italazimu mas'ala hizi zisiwe na hukumu za kisheria, lau kusingejitokeza maswali kutoka kwa watu kuhusiana nazo. Je matokeo ya uelewa kama huu ni sahihi?!!

**Hivi Aali - yaani Aali Muhammad - ni nani hao?!!**

Katika madrasa ya Ahlul'Bayt (a.s.) kwa maamuzi ya kukata shauri kabisa ni kuwa Aali waliokusudiwa katika swala, wao ni: Walio ma'asum miongoni mwa Ahlul-Bayti wake (s.a.w.w.) kwa kuwa kuswaliwa si wajibu kwa -asiyekuwa Mtume – na wao. [8]

7. *Al'Mugniy li'Ibni Quddaama* Juz. 1, uk. 581. *Al'Shar'hul'kabiiru* Jz. 1, uk. 581 kwa pambizo ya al'Mughniy, Chapa ya Darul kutaabu al'arabiy.

8. *Tadhkiratul'fuqahai* Juz. 3, uk. 234.

Na maamuzi haya yanashabihiana mno kuwa ni dharura miongoni mwa dharura za madhehebu hii ambazo zinajitosha hazihitajii uthibitisho, na zaungwa mkono na makumi ya Hadithi zilizoelezwa kutoka vyanzo vya kisunni kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.). Mfano wa *Musnad* ya Ahmad na *Al'Mustadraq ala Swahihayni*, *Al'Durul'manthur* ya Suyutiy, *Kanzul'ummal* na *Majmauz zawaidi.* Zote zajulisha kuwa Aali Muhammad (s.a.w.w.) ni Fatima, Ali na Hasan na Husein.[9]

Miongoni mwa hizo ni zile alizoeleza Imamu Ahmad katika *Musnad* yake, kuwa (s.a.w.w.) aliwakusanya pamoja Fatima, Ali, Hasan na Husein, na aliwafunika kishamia, kisha aliweka mkono wake juu ya kishamia akasema:

**اللهم ا ن هؤلاء أ ل محمد فا جعل صلوا تك و بر كاتك على محمد و ال محمد ا نك حميد مجيد"**

"Ewe Allah, kwa kweli hawa ni Aali Muhammad jaalia swala = yaani ghofrani na rehma zako na baraka zako zimfikie Muhammad na Aali Muhammad kwa kuwa wewe ni mwenye sifa tukufu u mtukufu. [10]

Pamoja na wingi wa Hadithi hizi na uwazi wake, zinalifanya suala hili kuwa linajitosheleza, yaani halihitajii kufanyiwa utafiti, ila tu tunajikuta pamoja na yote hayo zinajitokeza tafsiri za ajabu zinazosema kuwa eti wao, yaani Aali Muhammad ni: Wafuasi wake, au umma wake, au wafuasi na jamaa zake na watu wa ukoo, na kuna kauli isemayo: Ni kaumu yake, na imesemwa: Ahali wake walioharamishiwa swadaqa…

Na inakuja katika madhehebu ya al'Hasan kuwa mradi wa Aali ni Muhammad mwenyewe! Na hii ni rai ya ajabu mno!!

Na kuna walioitafasiri Aali Muhammad kuwa ni Bani Hashim. [11]

9. Al'mar'humu Al'Fayruzu Abadi alichukua jukumu la kukusanya sehemu ya Hadithi hizi katika kitabu chake *Fadhwailul'khamsa minaswihahi* sita Juz. 1, uk. 219-222.

10. *Musnad* ya Ahmad, Juz. 6. uk. 323.

11 As-Sawaiqul'Muhriqa: uk. 225. Pia angalia Al'Maj'mau ya an'Nawawiy Juz. 3, uk. 466 Chapa ya Darul'fikri .

Na lenye ubora ambalo tunahitimishia nalo utafiti huu katika nukta hii ni alilolisema al'Fakhru Raziy ndani ya tafsiri yake Al'Kabiir. Ameandika akisema: "Na mimi nasema: Aali Muhammad (s.a.w.w.) ni ambao jambo lao hurejea kwake. Na kila ambao jambo lao kwake ni lenye mkazo na kamili mno wao wanakuwa Aali. Na endapo tutalibebesha – Aali – kwa umma ambao umekubali da'awa yake wao pia ni Aali. Hapana shaka kuwa kwa Fatima, Ali, Hasan na Husein, (a.s.) ulikuwa muambatano kati yao na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ni muambatano wenye mkazo sana. Na hili ni kama lijulikanalo kwa nukuu fululizi kwa hiyo imewajibika wawe wao ndio al'Aali. Na tukilibebesha juu ya umma uliokubali da'awa yake kwamba wao pia ni Aali, kwa hiyo imethibiti kwa makadirio yote wao ndio al'Aali.

Ama watu wengine wasiokuwa wao je wanaingia chini ya tamko la al'Aali? Kuna tofauti.

Bwana mwenye tafsir ya al'Kashaafu ameeleza kuwa: "Ilipoteremka Aya hii - anaikusudia Aya ya ***Mawadda*** – palisemwa: Ewe Mtume wa Mungu: Nani hao wa karibu yako ambao mapenzi yao yamekuwa wajibu juu yetu?" Akasema: Ni Ali, Fatima, na watoto wao wawili." Ikathibiti kuwa hao wanne ndio makaribu wa Nabii (s.a.w.w.) Hili likithibiti inakuwa wajibu wao wawe waliofanywa makhsusi kwa taadhima, na hilo lajulishwa na sababu kadha.

Na sababu ya pili ambayo Al'Fakhru Raziy ameitaja ni:

**ا ن الدعاء للا ل منصب عظيم ولذلك جعل هذا الدعاء خاتمة التشهد فى الصلاة, وهو قوله(اللهم صلى على محمد وأل محمد و ارحم محمدا و أل محمد) وهذا التعظيم لم يوجد فى حق غير الا ل (**

"Kuwa dua kwa ajili ya al'Aali ni cheo adhimu, kwa minajili hiyo ameifanya dua hii hitmisho la ***tashahudi*** katika swala, nayo ni kauli yake: "Allahumma swali ala Muhammadin wa Aali Muhammadin warham

Muhammadan wa Ali Muhammadin” Na taadhima hii haipo kwa ajili ya wasio kuwa al’Aali **12.**

Hii, na al’Fakhru Raziy ametilia mkazo ndani ya tafsir yake kuwa umbo la swala ya Nabii (s.a.w.w.) ni: اللهم صل على محمد وعلى أل محمد Allahumma swali ala Muhammadin wa ala Aali Muhammad…[13]

**Mas’ala ndani ya uwanja wa mashindano ya kifiqhi**

Mas’ala hii katika asli yake haina hitilafu. Kama ambapo hakuna hitilafu katika ubora wa kumswalia Nabii (s.a.w.w.) na kuwa ni mustahabu wakati wote, na kupatikana thawabu kwa ajili yake, kwa sababu ya kupatikana khabari nyingi kwa hilo kutoka njia za Sunni na za Shia, kama kauli yake s.a.w من صلى علي صلاة صلى الله عليه بها عشرا = Mwenye kuniswalia swala moja Mungu humswalia kwa ajili yake kumi. **14**

Ila tu hitilafu imejitokeza katika pande mbili:

Ya kwanza: Nini umbo la swala juu yake? Tumekwishamaliza utafiti katika hilo na ukweli umebainika katika hilo, nao ni kuwa kuwataja (Aali Muhammad s.a.w) wakati wa kumswalia ni jambo la kisharia bali linalotakiwa kwa Waislamu wote, na kuwa kuacha kuwataja katika swala ya Nabii (s.a.w.w.) inaifanya kuwa swala iliyokatwa kama *Nassu Nabawiy sharifu* ilivyobainisha.

**Wakati gani swala ya Nabii na Aali wake huwa wajibu? Hilo ndilo tulitafitilo hivi sasa**

*12. Tafsiyrul’ kabiiru* Juz. 27. uk. 166.

13. Rejea ile ya mwanzo - yaani ile namba (1).

*14. Al’Jaamiu li ??Ahkamil’Qur’an* Juz. 14, uk. 235.

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 12



Na hapana shaka kuwa Aya hii ina umbo la amri na kwa daraja ya mkazo. Kwa kuwa ilipotanguliza ( ا ن الله وملائكته يصلون على النبي... imeleta amri ya mkazo, tamko lake: يائيها الذين أمنوا صلوا عليه وسلموا تسليما

Na ni jambo linalokubalika kwa wanachuoni wa *Usuul*: Kuwa **Swigha* ya amri inajulisha wajibu. Na hili ndilo lililofanya liletwe swali lifuatalo: Wakati gani swala ya Nabii (s.a.w.w.) inakuwa wajibu?

Na hapa kumejitokeza rai nyingi Az'Zamakhshariy ambazo amezitaja ndani ya tafsir yake kama zifuatazo:

فا ن قلت الصلاة على رسول الله ( ص. ع. و) وا جبة أم مندوبة ا ليها؟=

"Ukisema kumswalia Mtume wa Mungu (s.a.w.w.) ni wajibu au ni Sunnah? Nitasema: Bali ni wajibu, na wametofautiana hali ya kuwa kwake wajibu.

Miongoni mwao kuna walioiwajibisha kila inapotajwa.

Na katika Hadithi: "***Man dhukirtu indahu falam yuswali alay'ya fadakhalan Nara fa'ab'adahu llahu*** = Ambaye nimetajwa mbele yake na hakuniswalia na akaingia motoni na Mungu akamuweka mbali"

Na yaelezwa kuwa aliulizwa: Ewe Mjumbe wa Mungu, umeiona kauli ya Mungu Mtukufu***:*** "***Ina llaha wa malaikatahu yuswaluna alan Nabiyyi***…) Alisema s.a.w: ***Hadha minal Ilmil maknuni. Walaw la annakum sa'altumuniy an'hu ma akhbar tukum bihi***.= Hii ni miongoni mwa elimu iliyofichwa, lau ninyi musingeniuliza nisingekupeni khabari yake."

* *Swigha***:** Umbo la tamko

***Inna llaha wakala bi malakeyni fala udhkaru inda abdin muslimin fayuswali alay'ya ila Qala dhanikal'malakani: ghafara llahu laka.Wa qala llahu wa malaikatuhu lidhaynikal'malakayni: Aamiin"***=Kwa kweli Mungu ameniwakilishia malaika wawili, hivyo sitajwi mbele ya mja muislam na akaniswalia ila wale malaika wawili watasema: Mungu akusamehe. Na Mungu na malaika wake husema kuwajibu wale malaika wawili: Aamin).

Na miongoni mwao kuna aliyesema: Inakuwa wajibu katika kila kikao mara moja japo iwe imekaririwa kutajwa, kama ilivyosemwa katika Aya ya Sajda, na kumuombea rehma mtoa chafya, na kadhalika katika dua yote mwanzo wake na mwisho wake.

Na miongoni mwao kuna aliyewajibisha mara moja kwa umri, ni kama hivyo amesema katika kudhirisha Shahada mbili.

Na inavyolazimiana na ***ihtiyatu,*** yaani hadhari ni kumswalia kila atajwapo, kulingana na habari zilizopatikana.

Na endapo utasema: Kumswalia ndani ya swala je yenyewe ni sharti ya kuwa swala ni jaizi au hapana?

Nitasema: Abu Hanifa na swahibu zake hawaioni kuwa ni sharti. Na kutoka kwa Ibrahim An'Nakh'iy: Walikuwa wanatosheka badala ya hiyo – anawakusudia Swahaba, kwa tashahudi nayo ni *assalaamu alayka ayyuhan Nabiyyu.*

Ama Shafii r.a ameijaalia kuwa ni shart…) **1**

Qurtubiy amesema ndani ya tafsir yake: ( ***wala khilafa fii anna aswalata***

14. *Al'Kashaafu* Juz. 3, u k. 557-558.

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 14



***alayhi fardhun fil'umri maratan wa fii kuli hiin minal'wajibati wujubu Sunanil'muakada alati la yasau tarkuha, wala yaghfaluha ila man la khayra fiihi. =*** Wala hakuna tofauti kuwa kumswalia ni faradhi mara moja katika umri na kila wakati, ni miongoni mwa wajibu uwajibikaji wa Sunna yenye kutiliwa mkazo, ambayo haifai kuiacha, wala haghafiliki nayo ila asiye na kheri yeyote.[15]

Na Ibn Hazmi amechagua ndani ya *al'Mahala* kuwa yenyewe ni wajibu katika umri mara moja, na inayozidi moja ni mustahabu. Na alimpinga Shafii kuiwajibisha kwake ndani ya swala kuwa hayo ni madai bila ya uthibitisho. Na amepinga kuwa ni wajibu zaidi ya mara moja.

Kwa kuwa ziyada zaidi ya mara moja hapana budi iwe kwenye mpaka wa idadi maalumu. Na hakuna njia ya kufanya hivyo kwa kuwa hakuna dalili ya idadi maalumu [16]

Na hiyo pia ni rai ya al'Jaswasu. [17]
Na rai ya Shafi'iy: Yenyewe ni wajibu katika Tashahudi ya mwisho tu. Suala ni hivyo hivyo kwa Mahambaliy. Na wameitolea dalili kwa sababu nyingi. [18]

Ama madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s.) ni miongoni mwa yaliyo wazi mno kuwa ni wajibu kumswalia Nabii (s.a.w.w.) katika Tashahudi mbili zote. Sheikh Tusi ametoa dalili kuwa ni ( Ijmai ya kikundi hiki, na ni njia ya *Ihtiyatu,* kwa kuwa hapana tofauti kuwa akifanya hivyo Swala yake imepita. Na haijulishi kuwa iko sahihi endapo hatofanya hiyvo. Na pia kauli yake (s.w.t.): ( ***Ya'ayyuha ladhiyna a'amanu swaluu alayhi wa salimu tasliiman***) Na hii ni amri ya kumswalia yabidi iwe wajibu na wala hapana

15 *Al'Jaamiu liahkamil'Qur'an* Juz. 14 uk. 232- 233.

16 *Al'Mahala* Juz.3 uk.273.

*17 Ahkamul'Qur'an* Juz. 3, uk. 484. ) 4

18 *Al'Fiqhu alal'madhahibil'arba'a* Juz. 1Uk. 236,367. Pia angalia *Al'Mughniy* ya Ibnu Quddama al'Muqadasiy1:579-580.

mahali bora kuliko mahali hapa) kisha alieleza riwaya tatu zinazo julisha kuwa yenyewe ni wajibu katika swala

Ya kwanza kutoka kwa Ka'abu bin Aj'zata kutoka kwa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)

Na ya pili kutoka kwa Aisha kutoka kwa Mtume wa Mungu (s.a.w.w.)

Na ya tatu kutoka kwa Abu Baswiir kutoka kwa Imam Swadiqu (a.s.) [19]

Na katika *Tadhkiratul'fuqahai:* Imeelezwa kuwa amri ni ya wajibu na si wajibu nje ya Swala wa Ijmai. Kwa hiyo ni wajibu humo, na kwa kuwa Aisha alisema: "Nilimsikia Mtume wa Mungu s.a.w akisema: 'Swala haikubaliwi ila kwa tohara, na kwa kuniswalia.'

Na kwa kauli ya al'Swadiqu (a.s.) (***Man swala walam yuswali alan Nabiyyi s.a.w wa tarakahu amdan fala swalata lahu***= "Mwenye kuswali na hakumswalia Nabii (s.a.w.w.) na ameiacha maksudi, basi hana Swala.[20]

## CHUMO LA UTAFITI

Imepatikana kutokana na hayo kuwa swala ya Nabii (s.a.w.w.) yatakiwa kila wakati. Na kwamba yenyewe ni wajibu katika *Tashahudi* mbili za swala. Kutokana na hayo kunabainika kubatilika swala ambayo haikupatikana ndanimwe swala ya Nabii s.a.w.

Kama pia imepatikana kuwa makusudi ya swala ya Nabii (s.a.w.w.) ni ile ambayo Ahlul'Bayt wake wametajwa pamwe na yeye. Na kuwa swala isiyokuwa na utajo wao, Nabii s.a w ameiita swala *batraau***,** na Mtume

19. *Kitabul'khilafu* Juz. 1 Uk.369-371.
20. *Tadhkiratul'fuqahai* Juz.3, uk. 232.

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 16



mwenyewe (s.a.w.w.) ameikataza.

Kwa minajili hiyo swala ya wajibu iliyo tupu bila ya kuwataja wao (a.s.) ni sawa na iliyo swaliwa bila ya utajo wa Nabii (s.a.w.w.) aslan.

Na hizo zote mbili zinahukumiwa kuwa ni batili, kama alivyosema Imam Shafi'i:

***Ya a'ala bayti Rasuuli llahi hubukum***
***Fardhun mina llah fil'Qur'an anzalahu***
***Kafa kum min adhwimil'qadri annakum***
***Man lam yuswali alaykum la swalata lahu (1)***

(1) *al'Swawaiqul'muhriqatu li'Ibn Hajar* 228 katika tafsiyri ya Aya (*Inna llaha wa malaikatahu yuswaluna alan Nabiyyi….)* na ameyatafsiri maneno ya Shafi'iy katika hizi beti mbili na kuyapa uwezekano wa makusudio yake: *La swalata swahihatan*. hivyo inaafikiana na kauli yake ya kuwa kuwaswalia Aali pamwe na Nabii ni wajibu katika swala. Na ameyapa uwezekano wa kuwa makusudi hapana swala kamili ni: hapana swala kamili ili iafikiane na kauli yake katika mas'al hii

Ama kuwataja wasiokuwa wao pamoja na yeye katika swala ni kujikalifisha kwa wazi kusiko na dalili. Na suala ni kama alivyosema Al'Fakhru Raziy katika kuwaswalia (a.s.) pamwe na yeye (s.a.w.w.) ni daraja yenye adhwama makhsusi kwa ajili yao mbali na watu wengine. Na si miongoni mwa kumswalia yeye endapo kuachwe kuwaswalia Aali na badala yake asalimiwe: *alayhi swalatu wasalam*, au: *swala llahu alayhi wasalama*, Kwa kuwa ya kwanza ni *swalatu batra'u* iliyo katazwa. Na ya pili kuongezea hivyo salamu hii haina dalili hapa.[21]

21. Kwa ubainifu zaidi na ufafanuzi angalia makala: *wasalimu tasliiman inqiyadan au takriman?!*
*Fil'adadi15 min majalatil'fikri'lislamiy lil'yusifiy al'Gharawiy*

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 17



## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 18



27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 19



58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali

87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 21



114. Iduwa ya Kumayili.
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 22



140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Kati ya Alama kuu za dini Swala ya Jamaa.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka katika Qur'an sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya Pili
161. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
162. Falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Huduma ya Afya katika Uislamu
164. Hukumu za Mgonjwa

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd 7/2/2011 10:46 AM Page 23



165. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein
166. Uislamu Safi
167. Majlis ya Imam Husein
168. Mshumaa
169. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
170. Uislam wa Shia
171. Amali za Makka
172. Amali za Madina
173. Uislamu na mfumo wa Jamii ya dini nyingi
174. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
175. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
176. Elimu ya Tiba za Kiislam Matibabu ya Maimamu
177. Falsafa ya Dini

# BACK COVER

Kitabu hiki kinazungumzia juu ya hitilafu zilizotokea juu ya maneno yanayosomwa katika kumswalia Mtume Muhammad SAW *(**S**wallallaahu **'A**layhi **W**a-aalih).* Baadhi ya wanavyuoni wanasema kwamba kumswalia Mtume ni kusema: *"Allaahumma swalli 'alaa Muhammad"* bila kuongeza kitu. Wengine wanasema kumswalia Mtume ni kusema: *"Allaahumma swalli 'alaa Muhammad wa Aali Muhammad"* kama utakaavyoona maelezo yake ndani ya kitabu hiki.

Sheikh wetu huyu amefanya utafiti wa kina juu ya suala hili na kuonyesha kwa uwazi na pasina shaka yoyote juu ya asili ya swala ya Mtukufu Mtume. Mwanachuoni huyu mtafiti ametumia vyanzo halisi na sahihi katika kulifikia lengo lake hili. Vyanzo hivyo si vingine bali ni Qur'ani na Sunna, pamoja na matukio ya kweli ya kihistoria, akili, mantiki na elimu.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**

**Alitrah Foundation**

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv.com

Katika mtandao: www.alitrah.info

kumsalia Nabia Check Lubumba.qxd  7/2/2011  10:46 AM  Page 25